1906 Yusufu Ally Mwangamila
1907 Yusuph D. S. Itf Bushra Y. Simbila
1908 Yusuph Mbaruku Nyembo
1909 Yusuph Sadallah Maganga
1910 Zablon Paulo Mantutu
1911 Zacharia Majula Ekelege
1912 Zachariah Francis Mbata
1913 Zachariah Francis Mbata Itf Wisdom Zachariah Mbata
1914 Zahoro Mbwana Bingwe
1915 Zainab Karama
1917 Zaituni Haruni Kweka
1918 Zakia Atilio Mkembela
1919 Zan Securities Limited
1920 Zanzibar Social Security Fund
1921 Zedekia Ibrahim Ntulu
1922 Zena Nassoro Kadyyanji(Admin) Isaac
1923 Zennah S. Salimin
1924 Zephania Ole Megiroo Mollel
1925 Zerubabel Fathael Makundi
1926 Ziada Hamisi Sangaya
1927 Zuhura Kamwavi Mwale
1928 Zulfikar Esmail Nanji
1929 Zulfikar Nanji
1930 Zuya A.M.C.S. Ltd

1.0 KUFUNGUA MKUTANO MKUU

Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu, Dkt. Ally Hussein Laay alifungua Mkutano Mkuu saa 3:10 asubuhi baada ya akidi inayotakiwa kufikiwa. Hadi Mkutano Mkuu unafunguliwa, asilimia 71 ya hisa zote za Benki zilikuwa zimewakilishwa.

2.0 KURIDHIA DONDOO ZA MKUTANO MKUU

Wajumbe walipitisha dondoo za Mkutano Mkuu wa Ishirini na Tisa kama zilivyoainishwa kwenye ajenda ya Mkutano Mkuu.

3.0 KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA NANE

3.1 Wanahisa walipitisha Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Ishirini na Nane baada ya marekebisho yafuatayo kufanyika kwenye matokeo ya uchaguzi wa wajumbe huru wa Bodi:

3.2 Matokeo ya uchaguzi wa Wajumbe Huru wa Bodi

Na.	Jina la Mgombea	Idadi ya kura	Asilimia
1.	Prof. Neema Munisi Mori	1,678,122,338	97.98
2.	Eng. Boniface Gissima Nyamo-Hanga	34,557,277	2.02
Jumla		**1,712,679,615**	**100**

Na.	Jina la Mgombea	Idadi ya kura	Asilimia
1.	Ms. Miranda Naiman Mpogolo	1,516,367,075	90.13
2.	Ms. Joyce Nkini Iwisi	166,041,497	9.87
Jumla		**1,682,408,572**	**100**

3.3 Prof. Neema Munisi Mori na Bi. Miranda Naiman Mpogolo walichaguliwa kuwa Wajumbe Huru wa Bodi baada ya kupata idadi kubwa ya kura zilizopigwa kuliko wagombea wengine.

3.4 Mwenyekiti aliwaomba Wanahisa wenye maoni, marekebisho ya majina au majina yao kutokuwemo kwenye orodha ya waliohudhuria Mkutano Mkuu wawasilishe kwa Katibu.

3.5 Mwenyekiti na Katibu waliweka saini kwenye Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Ishirini na Nane.

4.0 KUJADILI YATOKANAYO NA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA NANE

4.1 KUIDHINISHA GAWIO KWA MWAKA 2022

Gawio la shilingi 45/= kwa hisa kwa mwaka ulioisha tarehe 31 Desemba, 2022 lililipwa kwa kila mwanahisa aliyekuwemo kwenye daftari lilipofungwa tarehe 9 Mei 2023 na malipo yalifanyika kuanzia tarehe 5 Juni, 2023.

4.2 KUIDHINISHA ADA YA WAKURUGENZI

Ada ya shilingi 965,000,000/= ililipwa kwa Wakurugenzi wa Bodi na wajumbe wa kamati nne za Bodi ya Wakurugenzi zilizopo sasa.

4.3 KUTEUA WAKAGUZI WA NJE WA HESABU

Kampuni ya Ukaguzi wa Hesabu ya *Ernst and Young* Tanzania ya S.L.P 2475, Dar es Salaam, iliteuliwa kuwa Wakaguzi wa Nje wa Hesabu za Benki na Kampuni zake Tanzu kwa mwaka 2023 kwa masharti na ada iliyopangwa na Bodi ya Wakurugenzi.

4.4 KUPANGA MAHALI NA TAREHE YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA TISA

Mkutano Mkuu wa Ishirini na Tisa wa Wanahisa wa Benki ya CRDB ulifanyika siku ya Jumamosi tarehe 18 Mei, 2024 katika kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC), kwenye ukumbi wa Simba kuanzia saa 3.00 kamili asubuhi kama ilivyoazimiwa.

5.0 KUJADILI NA KUPOKEA TAARIFA YA WENYE DHAMANA YA UONGOZI NA TAARIFA YA HESABU ZILIZOKAGULIWA KWA MWAKA ULIOISHA TAREHE 31/12/2023

5.1 TAARIFA YA WENYE DHAMANA YA UONGOZI

Mwenyekiti wa Bodi, Dkt. Ally Hussein Laay, aliwasilisha taarifa hiyo kama ifuatavyo:

Muhtasari wa Mazingira ya Uendeshaji

5.1.1 Mwaka 2023 uchumi wa dunia uliyumba na ukuaji wake ulishuka kutoka asilimia 3.5 mwaka 2022 hadi asilimia 3 na inatarajiwa utaendelea kushuka hadi asilimia 2.9 mwaka 2024. Hali hii ilisababishwa na; sera za fedha za kubana uchumi, migogoro ya kimataifa, hali mbaya ya hewa, na kushuka kwa ukuaji wa uchumi wa China. Mataifa kadhaa hasa wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), yalishuhudia mfumuko wa bei ukipanda na kuvuka viwango vya ukomo vilivyotarajiwa.

5.1.2 Licha ya changamoto zote hizi, uchumi wa Tanzania uliendelea ulikua kwa kasi ya kuridhisha hali iliyodhihirisha uimara wa Uchumi. Ukuaji huo ulichangiwa na ufanisi kwenye sekta ya kilimo, usafirishaji na uhifadhi wa bidhaa, pamoja na huduma za fedha na bima.

Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2023-2027)

5.1.3 Wajumbe walifahamishwa kwamba mwaka wa fedha 2023 uliweka msingi wa utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2023-2027) ambao umelenga kuboresha, kukuza na kuongeza huduma ndani na nje ya nchi. Mpango Mkakati huu ni wa muda wa kati na unajulikana kwa neno la Kiingereza 'EVOLVE' na umezingatia mafanikio yaliyopatikana kipindi kilichopita, maeneo ya maboresho pamoja na changamoto zilizokuwepo.

Pendekezo la Gawio

5.1.4 Bodi ilipendekeza kuidhinishwa kwa gawio la shilingi 50 kwa kila hisa moja kwa mwaka wa fedha ulioisha tarehe 31 Desemba 2023. Jumla ya gawio iliyo pendekezwa ilikuwa shilingi bilioni 130.6 sawa na asilimia 34 ya faida halisi iliyopatikana ikiwa ni ongezeka kutoka shilingi bilioni 117.5 zilizolipwa mwaka wa fedha 2022.

Malengo ya Baadaye

5.1.5 Benki itaendelea kubadilika kuendana na mabadiliko ya kibiashara yanayotokea ndani na duniani pamoja na utekelezaji wa miradi endelevu ikiwemo ***Kijani Bond*** (Hati Fungani ya Kijani).

5.1.6 Mojawapo ya vipaumbele vya Benki ni kuongeza thamani ya muda mrefu, kuwa Benki kiongozi na kuleta mabadiliko chanya na mafanikio makubwa kwa wadau na jamii.

Shukrani

5.1.7 Mwenyekiti aliwashukuru wafuatao

(i) Wanahisa kwa maoni yao

(ii) Wateja kwa kutumia huduma za Benki

(iii) Wafanyakazi na uongozi kwa bidii na kujituma

(iv) Bodi ya Wakurugenzi kwa miongozo kwa menejimenti

(v) Washirika, wazabuni, na mamlaka za usimamizi na udhibiti kwa kuendelea kuunga mkono Benki katika kila hatua.

(vi) Mamlaka na taasisi za serikali kwenye nchi zote ambako Benki inafanya biashara.

5.2 TAARIFA YA AFISA MTENDAJI MKUU

Afisa Mtendaji Mkuu, Bw. Abdulmajid Mussa Nsekela, aliwasilisha taarifa ya utendaji wa Benki kama ifuatavyo:

Ufanisi Katika Utendaji wa Benki ya CRDB

5.2.1 Benki ilitumia vema fursa zilizojitokeza sokoni na hivyo kufanikiwa kupata faida baada ya Kodi ya shilingi bilioni 422.8 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 20.3 kutoka faida ya shilingi bilioni 351.4 iliyopatikana mwaka 2022. Benki imejipanga kuhakikisha ongezeko la faida linakuwa endelevu kwa kuendelea kuwekeza kwenye kila fursa inayojitokeza pamoja na kutekeleza mipango ya mabadiliko.

5.2.2 Mchango wa kampuni tanzu kwenye Faida Baada ya Kodi ya Benki ulikua kwa asilimia 6, hali inayoonyesha uwezekano wa kuongezeka kwa faida hapo baadaye. Faida ya Kampuni tanzu ya CRDB Bank Burundi S.A. iliongezeka kwa asilimia 30.7 kufikia shilingi bilioni 30.2. Kampuni tanzu ya CRDB Insurance Company Limited ilipata hasara ya shilingi bilioni 1.7 na CRDB Bank Congo S.A. ilipata hasara ya shilingi bilioni 4.2. Kampuni hizi zilipata hasara kutokana na gharama kubwa za uanzishwaji kitu ambacho ni cha kawaida kwa kampuni changa. Inatarajiwa kwamba kampuni hizi zitaaanza kutengeneza faida katika kipindi kisichozidi miaka miwili ijayo.

Upanuzi wa Kikanda

5.2.3 Benki imetoa kipaumbele kwenye uwekezaji wa masoko mbalimbali kwa sasa kama vile Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). Umuhimu wa kimkakati wa DRC kwa Tanzania, pamoja na uhusiano wa kudumu kati ya mataifa hayo mawili, unatoa fursa ya kuvutia kwa Benki ya CRDB. Kuanzishwa kwa mafanikio kwa kampuni tanzu nchini DRC ni hatua ya kupongezwa licha ya changamoto zinazojitokeza. Mkakati huu makini wa upanuzi, pamoja na mwelekeo wa kuimarisha shughuli za ndani, unasisitiza maono ya kimkakati. Lengo kuu ni kupanua wigo wa kikanda na kutoa huduma bora, na hivyo kuhakikisha kutoa thamani endelevu kwa wadau wote kwa muda mrefu.

Maboresho ya miundo mbinu na mageuzi ya kidijitali

5.2.4 Benki iliendelea kuwekeza kimkakati kwenye TEHAMA kufanikisha malengo yake ya muda mrefu na wakati. Matumizi ya TEHAMA na chaneli za kidijitali yamesaidia shughuli nyingi za huduma za kibenki kufanyika kidijitali, hivyo kuongezeka ufanisi, na kushuka kwa gharama za utoaji huduma. Kutokana na hatua hizi uwiano wa gharama na mapato uliendelea kuwa asilimia 49.5, ambayo inakidhi kiwango elekezi kwa mujibu wa kanuni, ambacho kinatakiwa kuwa chini ya asilimia 55.

5.2.5 Benki ya CRDB imepiga hatua kubwa zilizochochewa na uwekezaji wa kimkakati katika mageuzi ya kidijitali, ambayo ni nguzo muhimu ya mkakati wa ukuaji. Benki imedhamiria kuimarisha miundombinu yake ya kiteknolojia na kuendeleza nguvu kazi yenye ujuzi wa kutosha kusukuma mabadiliko yenye athari chanya. Lengo kuu, kama lilivyoainishwa kwenye mkakati wa muda wa kati wa 2023-2027, ni kuboresha huduma kwa wateja ili kufikia ufanisi wa juu. Mwaka 2023, benki ilipiga hatua kubwa katika utekelezaji wa mradi wa mfumo mkuu mpya wa uendeshaji wa benki (CBS) na mfumo unganishi wa huduma (EBS), huku ikiimarisha uwezo wa kiteknolojia. Katikati ya mazingira yanayoendelea ya kiteknolojia, Benki ya CRDB inabaki imara katika kutafuta fursa zinazotokana na teknolojia ya Akili Mnemba (AI) na Uchambuzi wa Takwimu ili kuboresha ufanisi wa uendeshaji. Mtazamo wetu wa kimkakati ni kutumia teknolojia hizi za mageuzi kubuni huduma, kusaidia usimamizi wa vihatarishi kwa kutambua mitindo ya usalama wa mtandaoni, kuimarisha ufanisi wa uendeshaji kupitia uchambuzi katika mchakato wa utoaji wa mikopo, na kutekeleza mipango ya masoko kwa kuzingatia a tabia za wateja.

Uwekezaji kwenye raslimali watu

5.2.6 Mkakati mpya wa Benki wa muda wa kati unasisitiza umuhimu wa kukuza nguvu kazi inayoendana na mabadiliko, jitihada zinazoonekana kupitia mipango ya kina ya uboreshaji na usasishaji wa zana zinazolenga kukuza ubora wa utendaji unaodumu. Benki ilijielekeza katika maeneo matatu muhimu: ustawi wa wafanyikazi, ukuzaji wa taaluma na utambuzi wa wafanyikazi. Benki ina amini kwamba maeneo haya ni msingi wa kuunda nguvukazi yenye utendaji wa juu.

5.2.7 Katika kushughulikia ustawi wa wafanyakazi, Benki imetekeleza programu mbalimbali zinazosaidia uelewa wa afya ya akili na kimwili, pamoja na kuongeza msaada wa matibabu kwa wafanyakazi. Kuhusu maendeleo ya kazi, mipango imeanzishwa kuimarisha uwezo wa uongozi wa wafanyakazi wanawake, sambamba na ahadi yetu ya kutambua utofauti wa jinsia na kuhamasisha ujumuishi. Aidha, tumeanzisha jukwaa la kujifunza la kidijitali ili kuwezesha wafanyakazi kuongeza maarifa mara. Zaidi ya hayo, ili kuendeleza motisha na kukuza utamaduni wa kutambuliwa kwa wafanyakazi, tumerekebisha muundo wetu wa kutambua mchango wa wafanyazi kuendana na viwango vya sekta na kuunda mfumo thabiti wa motisha kwa wafanyakazi na maendeleo kazini.

Ushiriki wa Benki Katika Kutunza Mazingira

5.2.8 Benki ya CRDB inazingatia nguzo tano kutekeleza majukumu yake: Dunia, Watu, Utajiri, Ushirikiano, na Faida, ambazo zinaunganisha mazoea ya uendelevu katika mnyororo wa thamani. Benki ilitoa kipaumbele kwa ufadhili endelevu, kuhakikisha kuwa nguvu ya kifedha inakuwa chachu ya mabadiliko chanya ya mazingira na kijamii.

5.2.9 Benki inatambua athari za miradi ya kibiashara inayoitekeleza na jukumu lake la kuongoza kwa weledi na uadilifu. Benki iliendelea kutekeleza mpango wa kuhakikisha biashara yake haiathiri mazingira wala ustawi wa maisha ya watu.

5.2.10 Benki iliboresha usimamizi wa rasilimali, kupunguza utoaji wa gesi chafu, kuimarisha juhudi za kuchakata taka, na kudumisha kanuni za uwajibikaji za utoaji mikopo.

5.2.11 Benki iliwekeza katika mipango inayoleta thamani ya wadau na mustakabali endelevu ***(Environmental, Social and Governance- ESG)*** kwa kuweka mifumo ya uwazi na kina ya kuripoti taarifa za kifedha na zisizo za kifedha.

5.2.12 Benki iliendelea kubuni na kuwekeza katika matumizi ya kidijitali ambapo michakato ya utambuzi wa wateja kidijitali (e-KYC) na suluhuhisho zisizohitaji matumizi ya karatasi kama vile “OPTIMA” na “IPV,” zilianzishwa. Mifumo hii imesaidia Benki kupunguza athari ya shughuli zake kwenye mazingira.

5.2.13 Mafanikio ya kihistoria yalipatikana katika uzinduzi wa ***‘Kijani Bond,’*** ambayo ni hatifungani kubwa ya kijani katika ukanda wa Afrika Mshariki na Kati ambapo jumla ya shilingi bilioni 171 zilipatikana ikiwa ni zaidi ya lengo lililokusudiwa na hivyo kuthibitisha imani kubwa ya wawekezaji na dhamira ya Benki ya kutoa fursa za uwekezaji. Uwekezaji kupitia ***Kijani Bond*** utaelekezwa kwenye miradi inayozingatia utunzaji wa mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa, ikijumuisha nishati mbadala, miundombinu ya kijani, maji, nishati jadidifu, na kilimo kinachozingatia mabadiliko ya hali ya hewa.

5.2.14 Mwaka 2023 Benki ilianzisha kampuni itakayoendeleza mkakati wa kuiwezesha jamii kwenye miradi mbalimbali. Kampuni hii ijulikanayo kama ***CRDB Bank Foundation*** ni mahususi kwa ajili ya kufanikisha ufadhili wa miradi ya kuiwezesha jamii kuchangia mabadiliko chanya. Kupitia kampuni hii, Benki inakusudia kuchangia kwa kiasi kikubwa kwenye miradi ya elimu na huduma za afya.

Mtazamo wa Baadaye

5.2.15 Benki inatarajia kupata mafanikio zaidi katika biashara yake kwa kutoa kipaumbele kulinda biashara yake kuhakikisha uthabiti wa kifedha na kutoa huduma ya kipekee kwa wateja. Aidha, upanuzi wa njia za ufikishaji huduma kwa wateja na huduma za kidijitali utaimarisha uwepo wa Benki sokoni na kuongeza ushirikiano na wateja.

5.2.16 Benki itandelea kuboresha ushirikiano na Serikali, taasisi binafsi na mashurika ya fedha ya kimataifa kwa lengo la kuimarisha uwezo wake kimkakati, na maono ya wazi ya siku zijazo.

5.2.17 Uwezo wa menejimenti na wafanyakazi utaendelea kuboreshwa kwa lengo la kudumisha uongozi wake katika sekta ya benki, kukuza ustawi na maendeleo endelevu ndani na nje ya nchi. Benki itaendelea kuwekeza katika maendeleo ya teknolojia ili kupunguza hatari za mashambulizi ya mtandaoni na kuongeza kasi ya uvumbuzi wa kidijitali kuimarisha uwezo wa ushindani katika soko.

Shukrani

5.2.18 Afisa Mtandaji Mkuu aliwashukuru wafuatao:

(i) Wanahisa kwa kuendelea kuiamini na kuiunga mkono Benki.

(ii) Wateja, washirika, wazabuni, wadhibiti na wadau wengine.

(iii) Bodi ya Wakurugenzi kwa miongozo na kujitolea kwao katika kuhakikisha Benki inaendelea kuimarika kiutendaji.

(iv) Serikali na mamlaka za usimamizi na udhibiti kwa miongozo na ushirikiano wao thabiti.

(v) Menejimenti na wafanyakazi kwa kujitolea kwao kuendelea kuhakikisha kuwa ndoto za wanahisa zinatimia.

5.3 TAARIFA YA AFISA MKUU WA FEDHA

Afisa Mkuu wa Fedha, Bw. Frederick Bayona Nshekanabo, aliwasilisha taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa kama ifuatavyo:

Muhtasari wa Utendaji

5.3.1 Jumla ya mapato ya uendeshaji kabla ya uchakavu yaliongezeka kwa asilimia 16.3 kwa mwaka kutoka shilingi bilioni 1,112.9 mwaka 2022 hadi shilingi bilioni 1,294.3 Mafanikio hayo yalitokana na ongezeko la asilimia 17.6 katika mapato halisi yatokanayo na riba kutoka kwenye mikopo iliyotolewa kwa wateja wadogo, wa kati pamoja na ongezeko la mikopo yote iliyotolewa kwa ujumla. Mapato yatokanayo na miamala iliyofanyika kupitia ***SimBanking*** na huduma za benki kwa intaneti yaliongezeka na hivyo kuchangia ukuaji wa mapato..

5.3.2 Faida ya Benki baada ya kodi iliongezeka kwa asilimia 20.3 kutoka shilingi bilioni 351.4 mwaka 2022 hadi shilingi bilioni 422.8. Ukuaji huu unadhihirisha utekelezaji madhubuti wa mipango ya kimkakati na kuthibitisha azma ya Benki ya kukidhi matarajio ya wadau wake.

5.3.3 Kampuni tanzu ziliendelea kufanya vizuri na kuchangia kuimarisha utendaji wa Benki. Faida Baada ya Kodi iliyopatikana CRDB Bank Burundi S.A. iliongezeka kwa asilimia 30.7 na kufika shilingi bilioni 30.2. Thamani ya mali zake iliongezeka kwa asilimia 16.4 kwa mwaka huo hadi kufika shilingi bilioni 983.5 huku jumla ya amana za wateja ikiongezeka kwa asilimia 3.8 hadi kufika shilingi bilioni 547.3.

5.3.4 Kampuni tanzu mpya zilipata hasara; CRDB Insurance Company Limited ilipata hasara ya shilingi bilioni 1.7 na CRDB Bank Congo S.A. ilipata hasara ya shilingi bilioni 4.2. Inatarajiwa kwamba kampuni hizi zitaanza kutengeneza faida hivi karibuni na hivyo kukua na kuimarika kutokana na fursa nyingi zilizopo sokoni.

Gharama za Uendeshaji

5.3.5 Gharama za uendeshaji zilikua kwa asilimia 18.2 kutokana na juhudi za usimamizi bora wa matumizi. Gharama za wafanyakazi zilipanda kwa asilimia 10.9 hadi shilingi bilioni 338.2 kutokana na ongezeko la idadi ya wafanyakazi katika kampuni tanzu zilizoanzishwa ndani ya mwaka. Gharama za kiutawala ziliongezeka kwa asilimia 25.4 kufikia shilingi bilioni 218.6. Ongezeko hili lilichangiwa na mfumuko wa bei na kukua kwa biashara ikijumuisha kampuni mpya tanzu.

Mizania Imara

5.3.6 Mizania ya Benki ya CRDB na kampuni zake tanzu imeendelea kuimarika kufikia ukuaji wa mwaka wa asilimia 14.5 kutoka shilingi trilioni 11.6 mwaka 2022 mpaka shilingi trilioni 13.3 mwaka 2023.

5.3.7 Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na ongezeko la asilimia 22.8 la mikopo iliyotolewa hadi shilingi trilioni 8.4, ongezeko la amana za wateja zilizokua kwa asilimia 8.0, mikopo kwa asilimia 73.9 na kukua kwa mtaji wa wanahisa kwa asilimia 20.4.

Ubora wa Raslimali

5.3.8 Benki ilitekeleza mikakati ya kuhakikisha inakuwa na mikopo inayolipika na uwiano wa wateja unaotakiwa ***(Retail/Corporate ratio),*** ikiwa ni pamoja na kupunguza vihatarishi vinavyoambatana na mikopo, na kupata dhamana ya mikopo kwa kushirikiana na wabia wa kimkakati.

5.3.9 Benki ilimaliza mwaka ikiwa na uwiano wa mikopo chechefu wa asilimia 2.8 ambao uko ndani ya kiwango cha udhibiti cha asilimia 5. Urejeshaji wa mikopo mibaya uliongezeka kwa asilimia 172 kutoka shilingi bilioni 12.9 mwaka 2022 hadi shilingi bilioni 35.1

Hali ya Ukwasi

5.3.10 Benki ilikuwa na ukwasi wa kutosha kuwezesha ukuaji wa biashara zake. Uwiano wa ukwasi na mali ulikuwa asilimia 27 ikiwa ni kiwango cha juu ya ukomo wa kisheria wa asilimia 20.0.

5.3.11 Kampeni za uhamasishaji wa utunzaji wa amana zilichangia ukuaji wa asilimia 8.0 kwa mwaka hadi kufika shilingi trilioni 8.9, huku akaunti za hundi na akaunti za akiba zikiwa asilimia 83.0. Amana za wateja zilichangia asilimia 76.0 katika uwekezaji uliofanyika, mtaji ulichangia asilimia 14.9 na mikopo ilichangia asilimia 9.1.

Usimamizi wa Mtaji

5.3.12 Hadi tarehe 31 Desemba 2023, Benki ilikuwa na mtaji wa kutosha unaoiwezesha kukabiliana na changamoto au dharura inayoweza kujitokeza wakati wowote na kuendelea kukidhi vigezo vya kikanuni. Uwiano wa mtaji wa msingi ulikuwa asilimia 16 na uwiano wa jumla ya mtaji ilikuwa asilimia 17.3 hivyo kuwa juu ya matakwa ya kikanuni yanayotaka uwiano wa mtaji wa msingi uwe asilimia 12.5 na uwiano wa jumla ya mtaji kuwa asilimia 14.5 kwa benki za daraja la kwanza na daraja la pili.

Mtazamo wa Baadaye

5.3.13 Benki imelenga kuwapa faida kubwa zaidi wawekezaji wake inapoingia mwaka wa pili wa utekelezaji wa mpango mkakati wake wa miaka 5 (2023 – 2027). Benki itaendelea kuwa makini na shinikizo la mfumuko wa bei linaloongezeka katika uchumi wa dunia.

5.4 KUJADILI TAARIFA ZA WENYE DHAMANA YA UONGOZI, AFISA MTENDAJI MKUU NA HESABU ZILIZOKAGULIWA KWA MWAKA ULIOISHA DISEMBA 31, 2023

Wanahisa **WALIPOKEA** Taarifa za Wenye Dhamana ya Uongozi, Afisa Mtendaji Mkuu na Hesabu zilizokaguliwa na kuzijadili kama ifuatavyo:

5.4.1 **PONGEZI** zilitolewa kwa Bodi, Menejimenti na wafanyakazi kwa kufanya kazi kwa bidii na weledi na kuwezesha Benki kuendelea kupata faida kubwa na kupunguza mikopo chechefu, kuongeza gawio kwa wanahisa kila mwaka, kuandaa semina kutoa elimu kwa wanahisa na umma kuhusu masuala ya uwekezaji, kuanzisha programu ya IMBEJU kuwainua vijana na kina mama kiuchumi, jitihada za kuimarisha ujumuishwaji wa kiuchumi kwa kusaidia benki za kijamii na kuwekeza kwenye kilimo ili kukuza uchumi wa nchi.

5.4.2 Menejimenti **ILISHAURIWA** kwamba kwa kuwa mtaji wa Benki umekua kwa kiasi kikubwa, Bodi iangalie uwezekano wa kuongeza asilimia ya gawio inayotolewa kwa wanahisa kutoka asilimia 35 ya faida baada ya kodi inayotolewa hivi sasa. **ILIELEZWA** kwamba kiwango cha gawio kinachotolewa kwa wanahisa ni kwa mujibu wa Katiba ya Benki na kinazingatia mtaji na ukwasi wa Benki kuwezesha uwekezaji zaidi kuendelea kufanyika.

5.4.3 **ILISHAURIWA** kwamba Benki iendelee kuboresha ukwasi na mtaji wa Benki na kuchukua tahadhari kufanikisha mkakati wa Benki kupanua wigo wa huduma na bidhaa na kuongeza kampuni tanzu nje ya mipaka ya Tanzania. **ILIELEZWA** kwamba Benki inaendelea na mchakato wa kuangalia fursa bora na salama kwa ajili ya uwekezaji wenye tija ukanda wa kusini ya jangwa la Sahara na kwingineko.

5.4.4 **ILISHAURIWA** kwamba Benki iwekeze zaidi kwenye mifumo ya kidijitali kuboresha utoaji wa huduma kwa wateja na kuwa na njia mbadala pindi kukitokea hitilafu zinazoathiri huduma. **ILIELEZWA** kwamba Benki inaendelea kuwekeza katika mifumo ya kidijitali ambapo mwaka 2023, Benki ilipiga hatua ya kuridhisha katika utekelezaji wa mradi wa mfumo mkuu mpya wa uendeshaji wa benki (CBS) na mfumo unganishi wa huduma (EBS), huku ikiimarisha uwezo wa kiteknolojia katika kuboresha utoaji huduma kwa wateja.

5.4.5 **ILISHAURIWA** kwamba Benki iandae ***documentary*** kuonyesha mafanikio yake toka ilipoanzishwa hadi sasa kwa ajili ya kutunza historia na kumbukumbu kwa vizazi vijavyo. **ILIELEZWA** kwamba Benki inaandaa ***documentary*** itakayo akisi mafanikio ya Benki tangu ilipoanzishwa sambamba na maadhimisho ya miaka 30.

5.4.6 **ILISHAURIWA** kwamba Benki ijikite zaidi kutoa huduma vijijini ambako ndiko chimbuko lake na kuna mahitaji makubwa ya huduma hususan kwenye vyama vya ushirika. **ILIELEZWA** kwamba Benki inaendelea kuboresha huduma zake maeneo yote ya nchi ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya mawakala kupeleka huduma vijijini.

5.4.7 **ILISHAURIWA** kwamba Benki iboreshe utaratibu wa ushiriki wa wanahisa kwenye semina ya Uwekezaji pindi anapoalikwa kiongozi wa ngazi ya juu serikalini ambapo wanahisa huzuiwa kungia ndani hivyo kukosa nafasi ya kujifunza. **ILIELEZWA** kwamba utaratibu utaboreshwa kama ilivyoshauriwa. Mwenyekiti aliwaomba radhi wanahisa ambao walizuiwa kuingia ukumbini kutokana na ***sababu*** za ***kiprotokali***.

5.4.8 **ILISHAURIWA** kwamba kutokana na changamoto ya upatikanaji wa dola, nchi iangalie uwezekano wa kutumia dhahabu badala ya dola kufanya miamala kama ya uagizaji mafuta kutoka nje ya nchi. **ILIELEZWA** kwamba Serikali kupitia Benki Kuu imeendelea kuboresha upatikanaji wa dola kupitia mikakati mbalimbali kama vile kuhamasisha matumizi ya shilingi ya Kitanzania katika miamala mbalimbali hapa nchini na kuboresha sera na kanuni za uendeshaji wa maduka ya kuuza na kununua fedha za kigeni.

5.4.9 **ILISHAURIWA** kwamba Benki Kuu iangalie uwezekano wa kuondoa ukomo wa uongozi kwa wakurugenzi au watendaji wakuu wa Benki na taasisi nyingine za kifedha ambao wamethibitika kufanya kazi kwa waledi na kuchangia mageuzi na mafanikio makubwa ya taasisi hizo. **ILIELEZWA** kwamba ukomo wa muda wa uongozi wa watendaji wakuu wa benki zote nchini umeainishwa na Benki Kuu katika kanuni na miongozo ya utawala bora. Hivyo mabadiliko yake yanaweza kufanywa na Benki Kuu kwa kushirikiana na sekta ya fedha hapa nchini.

5.4.10 Mwenyekiti aliwashukuru Wanahisa kwa maoni yao na kuwahakikishia kuwa Bodi na Menejimenti watafanyia kazi maoni na ushauri waliotoa.

6.0 KUIDHINISHA GAWIO KWA MWAKA 2023

6.1 Bodi ya Wakurugenzi **ILIPENDEKEZA** gawio kwa mwaka ulioisha tarehe 31 Desemba, 2023 liwe shilingi 50/= kwa kila hisa kwa wanahisa waliokuwemo kwenye daftari lilipofungwa tarehe 13 Mei 2024 na malipo yafanyike kuanzia tarehe 5 Juni, 2024.

6.2 **ILIAZIMIWA** kwamba gawio kwa mwaka ulioisha tarehe 31 Desemba, 2023 liwe shilingi 50/= kwa kila hisa kwa wanahisa waliokuwemo kwenye daftari lilipofungwa tarehe 13 Mei, 2024 na malipo yafanyike kuanzia tarehe 5 Juni, 2024.

7.0 KUIDHINISHA ADA YA WAKURUGENZI

7.1 Bodi ya Wakurugenzi **ILIPENDEKEZA** jumla ya ada ya Wakurugenzi wa Bodi kwa mwaka 2024 iwe shilingi 965,000,000/= ambazo zitatumika pia kuwalipa wajumbe wa kamati nne za Bodi zilizopo sasa.

7.2 **ILIAZIMIWA** kwamba ada ya Wakurugenzi wa Bodi kwa Mwaka 2024 iwe shilingi 965,000,000 /= ambazo pia zitatumika kuwalipa wajumbe wa kamati nne za Bodi zilizopo sasa.

8.0 KUTEUA WAKAGUZI WA NJE WA HESABU

8.1 Bodi ya Wakurugenzi **ILIPENDEKEZA** Kampuni ya Ukaguzi wa Hesabu wa nje, PricewaterhouseCoopers (PWC) ya Dar es Salaam iteuliwe kuwa Wakaguzi wa Hesabu za Benki kwa mwaka 2024 kwa masharti na ada itakayopangwa na Bodi ya Wakurugenzi.

8.2 **ILIAZIMIWA** kwamba Kampuni ya Ukaguzi wa Hesabu wa nje, PricewaterhouseCoopers (PWC) ya Dar es Salaam iteuliwe kuwa Wakaguzi wa Hesabu za Benki kwa mwaka 2024 kwa masharti na ada itakayopangwa na Bodi ya Wakurugenzi.

9.0 KUCHAGUA WAJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI

9.1 Katibu aliwaeleza wanahisa kuwa kwa mujibu wa Katiba ya Benki, wajumbe wawili wa Bodi walitakiwa kujiuzulu. Wajumbe hao ni Prof. Faustine Karrani Bee anaewakilisha wanahisa wenye hisa chini ya asilimia moja na Bw. Gerald Paul Kasaato anaewakilisha wanahisa wenye hisa kati ya asilimia moja na kumi (1% na 10%). Prof. Bee na Bw. Kasaato waligombea kwa mara nyingine.

9.2 Wagombea wa nafasi ya Mjumbe wa Bodi anaewakilisha kundi la wanahisa wenye hisa chini ya asilimia moja walikuwa ni:

i. Prof. Faustine Karrani Bee
ii. CPA Oswald M. Urassa

9.3 Mgombea wa nafasi ya Mjumbe wa Bodi anaewakilisha wanahisa wenye hisa kati ya asilimia moja na kumi (1% na 10%) alikuwa ni Bw. Gerald Paul Kasaato.

9.4 Katibu alitoa maelezo jinsi ya kupiga kura kidijitali na uchaguzi ulifanyika kama ilivyopangwa. Wanahisa walipiga kura kuwachagua wajumbe wa Bodi kulingana na kundi lao.

9.5 Matokeo ya uchaguzi wa Mjumbe wa Bodi anaewakilisha wanahisa wenye hisa chini ya asilimia moja

No.	Jina la Mgombea	Idadi ya kura	Asilimia
1.	Prof. Faustine Karrani Bee	215,481,599	60.45
2.	CPA Oswald M. Urassa	140,998,024	39.55
Jumla		**356,479,623**	**100**

9.6 Matokeo ya Uchaguzi Mjumbe wa Bodi anaewakilisha wanahisa wenye hisa kati ya asilimia moja na kumi (1% na 10%).

No.	Jina la Mgombea	Idadi ya kura	Asilimia
1.	Gerald Paul Kasaato	479,291,134	100
Jumla		479,291,134	**100**

9.7 Mwenyekiti alimtangaza Prof. Faustine Karrani Bee kuwa Mjumbe wa Bodi anaewakilisha wanahisa wenye hisa chini ya asilimia moja baada ya kupata idadi kubwa ya kura zilizopigwa.

9.8 Mwenyekiti alimtangaza CPA Oswald M. Urassa kuwa kwenye orodha ya akiba.

9.9 Mwenyekiti alimtangaza Bw. Gerald Paul Kasaato kuwa Mjumbe wa Bodi anaewakilisha wanahisa wenye hisa kati ya asilimia moja na kumi (1% na 10%).

9.10 Prof. Bee aliwashukuru Wanahisa kwa kumchagua kwa kipindi kingine cha miaka mitatu na kuwaahidi kuwa ataendelea kutekeleza majukumu yake akishirikiana na wajumbe wengine wa Bodi kutoa miongozo itakayosaidia Benki kuwa na mafanikio zaidi.

9.11 Bw. Kasaato aliwashukuru Wanahisa kwa kumpa nafasi nyingine ya kuwa Mjumbe wa Bodi na kuahidi kufanya kazi kwa bidii zaidi kwa kushirikiana na Wajumbe wengine wa Bodi ili kuongeza ufanis wa utendaji wa Benki.

10.0 KUJADILI MAPENDEKEZO KUTOKA KWA WANAHISA

Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu alitangaza kuwa hakuna mapendekezo yaliyopokelewa kutoka kwa wanahisa.

11.0 MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI

Hayakuwepo mengineyo kutoka kwa Wanahisa.

12.0 KUPANGA MAHALI NA TAREHE YA MKUTANO MKUU WA THELATHINI

12.1 Bodi ya Wakurugenzi **ILIPENDEKEZA** Mkutano Mkuu wa Thelathini wa Wanahisa wa Benki ya CRDB Plc ufanyike siku ya Jumamosi tarehe 17 Mei, 2025 katika kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC), Ukumbi wa Simba kuanzia saa 3.00 kamili asubuhi.

12.2 **ILIAZIMIWA** kuwa Mkutano Mkuu wa Thelathini wa Wanahisa wa Benki ya CRDB ufanyike siku ya Jumamosi tarehe 17 Mei, 2025 katika kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC), Ukumbi wa Simba kuanzia saa 3.00 kamili asubuhi.

13.0 KUFUNGA MKUTANO

13.1 Mwenyekiti aliwashukuru wanahisa na wadau kwa kuhudhuria Mkutano Mkuu na kuahidi kuwa maoni na masuala yote yaliyowasilishwa na wanahisa yatafanyiwa kazi na Menejimenti.

13.2 Alitoa shukrani kwa Benki Kuu ya Tanzania, Mamlaka ya Masoko na Mitaji (CMSA) na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) kwa usimamizi na kutoa miongozo kwa maendeleo ya sekta ya Benki na masoko ya mitaji.

13.3 Aliwashukuru wajumbe wa Bodi na kuwakaribisha tean wajumbe wa Bodi waliochaguliwa. Alimpongeza mgombea wa nafasi ya ujumbe wa Bodi ambae kura hazikutosha.

13.4 Aliwapongeza wafanyakazi kwa mafanikio yaliyopatikana na kuwataka kuendelea kujituma ili kupata mafanikio makubwa zaidi.

13.5 Alipongeza sekretarieti kwa maandalizi mazuri ya Semina na Mkutano Mkuu.

13.6 Mwenyekiti alifunga Mkutano saa 9:15 alasiri.

IMETHIBITISHWA

_________________________ _________________________

MWENYEKITI **KATIBU**

____

TAREHE

Dondoo Na 4: **YATOKANAYO NA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA TISA WA WANAHISA WA CRDB BANK PLC ULIOFANYIKA JIJINI ARUSHA KATIKA KITUO CHA MIKUTANO CHA KIMATAIFA ARUSHA (AICC), UKUMBI WA SIMBA TAREHE 18 MEI 2024**

NO	KUMB	MAPENDEKEZO/USHAURI	UTEKELEZAJI
1.0	**6.0**	**KUIDHINISHA GAWIO KWA MWAKA 2023**	
1.1	**6.2**	**ILIAZIMIWA** kwamba gawio kwa mwaka ulioisha tarehe 31 Desemba, 2023 liwe shilingi 50/= kwa kila hisa kwa wanahisa waliokuwemo kwenye daftari lilipofungwa tarehe 13 Mei, 2024 na malipo yafanyike kuanzia tarehe 5 Juni, 2024.	Gawio la shilingi 50/= kwa hisa kwa mwaka ulioisha tarehe 31 Desemba, 2023 lilipwa kuanzia tarehe 5 Juni 2024 kama ilivyoazimiwa
2.0	**7.0 KUIDHINISHA ADA YA WAKURUGENZI**		
2.1	**7.2**	**ILIAZIMIWA** kwamba ada ya Wakurugenzi wa Bodi kwa Mwaka 2024 iwe shilingi 965,000,000 /= ambazo pia zitatumika kuwalipa wajumbe wa kamati nne za Bodi zilizopo sasa.	Ada ya Wakurugenzi kwa Mwaka 2024 ni shilingi 965,000,000 /= ambazo pia zitatumika kuwalipa wajumbe wa kamati nne za Bodi ya Wakurugenzi zilizopo sasa kama ilivyopendekezwa na Bodi ya Wakurugenzi..
3.0	**8.0 KUTEUA WAKAGUZI WA NJE WA HESABU**		
3.1	**8.2**	**ILIAZIMIWA** kwamba Kampuni ya Ukaguzi wa Hesabu ya Pricewaterhouse Coopers ya Dar es Salaam, iteuliwe kuwa Wakaguzi wa Nje wa Hesabu za Benki na Kampuni zake tanzu kwa mwaka 2024 kwa masharti na ada itakayopangwa na Bodi ya Wakurugenzi.	Kampuni ya Ukaguzi wa Hesabu ya PricewaterhouseCoopers ya Dar es Salaam ni Wakaguzi wa Nje wa Hesabu za Benki na Kampuni zake Tanzu kwa mwaka 2024 kwa masharti na ada iliyopangwa na Bodi ya Wakurugenzi.
4.0	**9.0 KUCHAGUA WAJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI**		
4.1	**9.5**	Mwenyekiti alimtangaza Prof. Faustine Karrani Bee kuwa Mjumbe wa Bodi anaewakilisha wanahisa wenye hisa chini ya asilimia moja na Bw. Gerald Kasaato kuwa Mjumbe wa Bodi anaewakilisha wanahisa wenye hisa kati ya asilimia 1 na asilimia 10 baada ya kupata idadi kubwa ya kura zilizopigwa kuliko wagombea wengine.	Wajumbe wote wa Bodi waliochaguliwa waliidhinishwa na Benki Kuu.
5.0	**12.0 KUPANGA MAHALI NA TAREHE YA MKUTANO MKUU WA THELATHINI**		
5.1	**12.2**	**ILIAZIMIWA** kwamba Mkutano Mkuu wa Thelethini (30) wa Wanahisa wa Benki ya CRDB ufanyike siku ya Jumamosi tarehe 17 Mei, 2025 katika kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC), Ukumbi wa Simba kuanzia saa 3.00 kamili asubuhi.	Mkutano Mkuu wa Thelathini (30) wa Wanahisa wa Benki ya CRDB umefanyika siku ya Jumamosi tarehe 17 Mei, 2025 katika kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC), Ukumbi wa Simba kuanzia saa 3.00 kamili asubuhi kama ilivyoazimiwa.

Bw. Abdulmajid M. Nsekela

MKURUGENZI MTENDAJI

Dondoo Na. 5 TAARIFA YA BODI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA YA HESABU ZILIZOKAGULIWA ZA MWAKA 2024

5.1 KUPOKEA TAARIFA YA BODI YA WAKURUGENZI

(Taarifa itaambatishwa)

Wanahisa wanaombwa kupitisha azimio la kuipokea taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi.

5.2 KUPOKEA TAARIFA YA HESABU

(Taarifa itaambatishwa)

Wanahisa wanaombwa kupitisha azimio la kuipokea taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2024.

5.3 GAWIO KWA MWAKA 2024

5.3.1 Pendekezo

Kwa mujibu wa kifungu namba 140 cha Katiba ya Kampuni, Bodi ya Wakurugenzi inapendekeza gawio kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Desemba 2024 liwe Shilingi 65/= kwa kila hisa kwa wanahisa watakaokuwepo kwenye daftari litakapofungwa tarehe 07 Mei 2025 na malipo yafanywe kuanzia tarehe 02 Juni 2025.

5.3.2 Kinachohitajika

Wanahisa wanaombwa kupitisha azimio la kuafiki pendekezo la Bodi ya Wakurugenzi kwamba gawio kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2024 liwe shilingi 65/= kwa hisa kwa wanahisa watakaokuwepo kwenye daftari litakapofungwa tarehe 07 Mei 2025 na malipo yafanyike kuanzia tarehe 02 Juni 2025.

Dondoo Na. 6 KUIDHINISHA ADA YA WAKURUGENZI WA BODI

6.1 Pendekezo

6.1 Kuidhinisha Ada ya Wakurugenzi

6.1.1 Bodi ya Wakurugenzi INAPENDEKEZA kwamba jumla ya ada ya Wakurugenzi wa Bodi kwa mwaka 2025 iwe shilingi 1,090,000,000/= ambazo zitatumika pia kuwalipa wajumbe wa kamati nne za Bodi zilizopo sasa.

6.1.2 Kinachohitajika: Wanahisa wanaombwa kuidhinisha jumla ya ada ya Wakurugenzi wa Bodi kwa mwaka 2025 ya shilingi 1,090,000,000/= ambazo zitatumika pia kuwalipa wajumbe wa kamati nne za Bodi zilizopo sasa.

Dondoo Na. 7 KUTEUA WAKAGUZI WA HESABU

7.1 Mapendekezo

Bodi ya Wakurugenzi, inapendekeza Kampuni ya Ukaguzi wa Hesabu wa nje, PriceWaterhouseCoopers (PWC) Dar es Salaam, iteuliwe kuwa Wakaguzi wa hesabu za Benki kwa mwaka 2025, kwa masharti na ada itakayopangwa na Bodi ya Wakurugenzi.

7.2 Kinachohitajika

Wanahisa wanaombwa kupitisha azimio la kuteua Kampuni ya Ukaguzi wa Hesabu wa nje, PriceWaterhouseCoopers (PWC) Dar es Salaam, kuwa wakaguzi wa Benki kwa mwaka 2025, kwa masharti na ada itakayopangwa na Bodi ya Wakurugenzi.

Dondoo Na. 8 MABADILIKO YA VIFUNGU NAMBA 88, 92, 94.2, 94.3 NA 167 VYA KATIBA YA BENKI.

8.0 Utangulizi:

Bodi ya CRDB Bank Plc inapendekeza marekebisho ya vifungu vya Katiba ya Benki (MEMARTS), kwa lengo la kuboresha utawala bora na michakato ya uendeshaji wa Benki. Marekebisho yanayopendekezwa yanahusu maeneo yafuatayo:

a) Uchaguzi wa Wajumbe wa Bodi: Mabadiliko ya taratibu za uteuzi na uchaguzi wa wakurugenzi, kuhakikisha mchakato wa uwazi zaidi, ufanisi, na usawa unaowiana na taratibu za utawala bora.

b) Ukomo wa Ujumbe wa Bodi: Kuoanisha Kanuni za Benki na Taasisi za Fedha (Utawala Bora) za 2021, ambazo zinaweka ukomo wa kuhudumu kwa wajumbe wa Bodi kuwa miaka 10. Benki kuruhusu ufikishaji wa taarifa mbali mbali kwa wanahisa kwa kutumia njia za kielektroniki na kidijitali.

c) Utumaji Notisi: Maboresho ya njia zinazotumiwa na Benki kufikisha taarifa kwa wanahisa, kuruhusu ufikishaji wa taarifa mbali mbali kwa wanahisa kwa kutumia njia za kielektroniki na kidijitali.


ustawi pamoja

1.0 Election of Board Members.

The Board is proposing amendments to Article 88, Article 92 and Article 94.2 and 94.3, specifically addressing the election and nomination of board members.

Current Wording	Proposed Changes
Article 88	
In the event the category holding less than 1% of the issued and fully paid-up share capital of the bank does not at all meet the 10% threshold, it shall be entitled to jointly elect one (1) Director only from a nomination list of candidates approved by the Board.	In the event that the category holding less than 1% of the issued and fully paid-up share capital of the Bank does not meet the 10% threshold, it shall be entitled to nominate and elect one (1) Director in accordance with Article 92.
Article 92	
The Governance, Nomination and Human Resources (HR) Committee shall on behalf of the Board prepare two nominees basing on the qualification needed by the Board for each seat of director sought who will be submitted to the annual general meeting for members under Articles 85, 87 and 88 for election.	The Board shall take such actions as are reasonably necessary to identify and attract the best candidates for directorship for the available positions on the Board. This will include advertising the positions in widely circulated news media within Tanzania. The Board shall then provide one candidate for each member under Article 85, 87 and 88 to the Annual General Meeting for the appointment of a director for members under Articles 85, 87 and 88.
Article 94.2 and Article 94.3	
94.2 In the case of other categories of members, the persons who was second in the election shall be appointed subject to approval by the Bank; and 94.3 In case all proposed appointees are not approved by the Bank, the appointment process shall commence afresh.	94.2 [To be deleted] [Following deletion of Clause 94.2, Clause 94.3 shall read as Clause 94.2]. 94.3 In the event the proposed candidate is not approved by the Bank, the position will remain vacant for the remainder of the year, and the appointment process shall commence afresh for the next Annual General Meeting, provided that the number of directors is not less than nine (9) as per Article 79.
Article 98	

Rationale for Changes
